
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA JUNI – AGOSTI (JJA), 2022



**Dondoo muhimu za hali ya hewa kipindi cha Juni-Agosti (JJA), 2022**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na hali ya hewa inayotarajiwa katika msimu wa Kipupwe katika kipindi cha Juni hadi Agosti (JJA), 2022; Ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa kawaida, kipindi cha miezi ya Juni hadi Agosti (JJA), huwa ni kipindi cha baridi na upepo kwa maeneo mengi ya nchi. Kwa muhtasari, mwelekeo huo kwa mwaka 2022 pamoja na athari zake unaonesha kuwa:

a) **Viwango vya joto**

- Katika kipindi cha JJA, 2022 hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani inatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki.

- Vipindi vya baridi zaidi vinatarajiwa kujitokeza mwezi Juni na Julai.

- Vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi.

**b) Upepo**

- Katika kipindi cha miezi ya Juni na Agosti, 2022 vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kushamiri katika maeneo mengi nchini. Msimu wa Juni hadi Agosti 2022 unatarajiwa kuwa na upepo utakaovuma kutoka kusini-mashariki na mashariki (Matlai) katika ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maeneo ya nchi kavu hususan mwezi Agosti, 2022.

c) **Athari**

- Magonjwa ya mifugo yanayoambatana na baridi kama vile homa ya mapafu yanaweza kujitokeza

- Hali ya vumbi inayoambatana na upepo mkali katika baadhi ya maeneo inatarajiwa kujitokeza na inaweza kuathiri afya ya binadamu na wanyama

## 1.0 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha msimu wa Kipupwe (Juni hadi Agosti), 2022, hali ya joto la bahari katika ukanda wa tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki inatarajiwa kuwa ya chini ya wastani. Hali ya joto la bahari la wastani inatarajiwa katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) na juu kidogo ya wastani katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi (Pwani ya Indonesia). Vilevile, joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la bahari kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola). Kwa ujumla hali hii inatarajiwa kusababisha hali ya ukavu katika msimu huu wa Kipupwe.

Kwa upande mwingine, joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo kubwa la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi (kusini-mashariki mwa Madagascar) na joto la bahari la wastani katika eneo la mashariki mwa baharí ya Hindi (magharibi mwa Australia) linatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kupunguza nguvu ya mgandamizo mkubwa wa hewa (Mascarine), kasi na uwepo wa vipindi vya upepo wa kusi na hali ya ubaridi kwenye maeneo mengi nchini hasa yale yaliyopo ukanda wa pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini-mashariki.

## 2.0 MATARAJIO YA VIWANGO VYA JOTO KWA MIEZI YA JUNI HADI AGOSTI, 2022

Katika kipindi cha JJA, 2022 hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani inatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi vya baridi zaidi vinatarajiwa kujitokeza katika mwezi wa Juni na Julai.

**2.1 Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Shinyanga na Simiyu):**
Kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kati *ya nyuzi joto 14* $^{o}$C *na 20* $^{o}$C katika maeneo mengi.

**2.2 Ukanda wa pwani ya kaskazini (Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**

Hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi. Kiwango hicho kinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto *22* $^{o}$C *na 26* $^{o}$C kwa maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na 18 $^{o}$C na 22 $^{o}$C katika maeneo ya nchi kavu. Hata hivyo, maeneno yenye miinuko hususan katika mikoa ya Tanga na Morogoro yanatarajiwa kuwa na kiwango cha *nyuzi joto* chini ya 18 $^{o}$C.

**2.3 Kanda ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi, kiwango hicho kinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto *10* $^{o}$C *na 18* $^{o}$C. Hata hivyo, maeneno yenye miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango cha *nyuzi joto* chini ya 10 $^{o}$C.

**2.4 Kanda ya magharibi (Mikoa ya Tabora, Rukwa, Katavi na Kigoma ):**

Hali ya baridi ya kawaida hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ambapo joto linatarajiwa kuwa kati ya *nyuzi joto 14* $^{o}$C *na 20* $^{o}$C.

**2.5 Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):**

Hali ya baridi ya kawaida hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ambapo joto linatarajiwa kuwa kati ya *nyuzi joto 12* $^{o}$C *na 18* $^{o}$C.

**2.6 Ukanda wa pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**


Hali ya baridi ya kawaida hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ambapo joto linatarajiwa kuwa kati ya *nyuzi joto 14* $^{o}$C *na 22* $^{o}$C.

**2.7 Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**


Hali ya baridi ya kawaida hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ambapo joto linatarajiwa kuwa kati ya *nyuzi joto 6* $^{o}$C *na 14* $^{o}$C.

**2.8 Kanda ya nyanda za juu kusini-magharibi (Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe pamoja na maeneo ya kusini ya mkoa wa Morogoro):**

Hali ya baridi ya kawaida hadi joto kiasi inatarajiwa katika maeneo mengi ambapo joto linatarajiwa kuwa kati ya *nyuzi joto 4* $^{o}$C *na 14* $^{o}$C. Hata hivyo, katika maeneo ya miinuko kiwango hicho kinatarajiwa kuwa chini ya nyuzi joto 4 $^{o}$C.




*Picha 1: Mwelekeo wa viwango vya joto la chini katika msimu wa JJA, 2022*




*Picha 2: Wastani wa muda mrefu wa viwango vya joto la chini kwa msimu wa Juni hadi Agosti.*

**3.0 MWENENDO WA UPEPO KWA KIPINDI CHA JUNI HADI AGOSTI (JJA), 2022**

Kwa kawaida msimu wa Kipupwe hutawaliwa na upepo wa Kusi. Hata hivyo, msimu wa Juni hadi Agosti 2022 unatarajiwa kuwa na upepo utakaovuma kutoka kusini-mashariki na mashariki (Matlai) katika ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi na maeneo ya nchi kavu hususan mwezi Agosti,2022. Kwa ujumla upepo mkali unatarajiwa kushamiri katika maeneo mengi nchini.

**4.0 ATHARI NA USHAURI**

Athari na ushauri kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao ni kama ifuatavyo.

**4.1 ATHARI:** Magonjwa ya mifugo yanayoambatana na baridi kama vile homa ya mapafu yanaweza kujitokeza. Vile vile, hali ya vumbi inayoambatana na upepo mkali katika baadhi ya maeneo inatarajiwa kujitokeza na inaweza kuathiri afya ya binadamu na wanyama.

**4.2 USHAURI**: Maji na malisho vitumike kwa uangalifu ili kukabiliana na upungufu unaotarajiwa kuendelea.

Tahadhari za kiafya zichukuliwe kujikinga dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na hali ya baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi. Wakulima wahimizwe kulima mazao ya mbogamboga na mizizi kama vile viazi kwenye maeneo oevu.

***Angalizo 1:*** *Licha ya hali ya ukavu ambayo inatarajiwa kuendelea katika msimu wa JJA 2022, upepo unaotarajiwa kuvuma kutoka kusini mashariki na mashariki unaweza kuleta unyevuunyevu kutoka Bahari ya Hindi na kusababisha vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani).*

**Angalizo 2:** *Mwelekeo wa hali ya hewa uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya hewa katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.*

***Imetolewa: 01 Juni, 2022.***

***Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)***